JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A (GATCE) 2023

## URAIA

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA

# TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KATIKA MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A (GATCE) 2023

# 612 URAIA

*Kimechapishwa na:*
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P 2624, Dar es Salaam, Tanzania.

© **Baraza la Mitihani la Tanzania, 2023**

Haki zote zimehifadhiwa.

## YALIYOMO

DIBAJI....................iv

1.0 UTANGULIZI .................... 1

2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KWA KILA SWALI .. 2

2.1 SEHEMU A: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI .................... 2

2.1.1 Swali la 1: Dola .................... 2

2.1.2 Swali la 2: Dola .................... 4

2.1.3 Swali la 3: Utamaduni Wetu .................... 6

2.1.4 Swali la 4: Uchumi wa Tanzania .................... 9

2.1.5 Swali la 5: Uchumi wa Tanzania .................... 11

2.1.6 Swali la 6: Misingi ya Ufundishaji wa Somo la Uraia. .................... 13

2.1.7 Swali la 7: Utamaduni Wetu .................... 16

2.1.8 Swali la 8: Zana Kufundishia na Kujifunzia .................... 19

2.1.9 Swali la 9: Maandalizi ya Kufundisha Somo la Uraia .................... 21

2.1.10 Swali la 10: Dola .................... 24

2.2 SEHEMU B: MASWALI YA INSHA .................... 26

2.2.1 Swali la 11: Uchambuzi wa Maandiko/Machapisho Muhimu ya Kufundishia /Kujifunzia Somo la Uraia .................... 26

2.2.2 Swali la 12: Upimaji na Tathmini .................... 31

2.2.3 Swali la 13: Maandalizi ya Kufundisha Somo la Uraia .................... 36

2.2.4 Swali la 14: Uchambuzi wa Maandiko/Machapisho Muhimu ya Kufundishia/Kujifunzia Somo la Uraia .................... 40

3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA MADA. 45

4.0 HITIMISHO .................... 46

5.0 MAPENDEKEZO .................... 46

Kiambatisho A .................... 47

Kiambatisho B .................... 48

## DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa ya uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika mtihani wa Cheti Daraja la A katika somo la Uraia mwaka 2023. Lengo la taarifa hii ni kutoa mrejesho wa ufaulu wa watahiniwa kwa walimu tarajali, wakufunzi, watunga sera, wakuza mitaala na wadau wengine wa elimu kuhusu namna watahiniwa walivyojibu maswali ya mtihani.

Taarifa imeeleza sababu za watahiniwa kufanya vizuri, wastani au vibaya katika mtihani huu. Kwa ujumla, ufaulu katika somo la Uraia ulikuwa wa kiwango kizuri kwani watahiniwa walitambua mahitaji ya maswali yaliyoulizwa, walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada husika, walielewa vizuri dhana mbalimbali zilizotahiniwa, walikuwa na uwezo wa kujibu maswali kulingana na nyanja husika na walikuwa na ujuzi wa kutosha katika uandishi wa insha. Vilevile, katika maswali yaliyokuwa na ufaulu wa wastani, watahiniwa walitoa hoja chache kuliko matakwa ya swali husika na wengine walirudia hoja moja kwa namna tofauti.

Hata hivyo, katika maswali yaliyokuwa na ufaulu hafifu, watahiniwa hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada zilizotahiniwa, dhana mbalimbali zinazohusiana na somo la Uraia na matakwa ya swali. Aidha, watahiniwa hao walikosa umahiri wa kujieleza katika mtiririko unaoleta mantiki na kushindwa kuandika sehemu za utangulizi na hitimisho hususan katika maswali ya insha.

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika maswali waliyojibu unatoa picha halisi ya mafanikio na changamoto zinazojitokeza katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Uraia katika vyuo vya Ualimu Tanzania.

Ni matumaini ya Baraza la Mitihani la Tanzania kuwa mrejesho huu utawawezesha viongozi wa elimu, wakuu wa vyuo, wakufunzi na wanavyuo kutumia mbinu muafaka ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Maboresho hayo yatasaidia kuinua kiwango cha ufaulu kwa watahiniwa katika mitihani inayoandaliwa na Baraza la Mitihani la Tanzania kwa wakati ujao.

Mwisho, Baraza la Mitihani la Tanzania linapenda kuwashukuru wote waliohusika katika uchambuzi wa takwimu na kuandaa taarifa hii.



Dkt. Said A. Mohamed

**KATIBU MTENDAJI**

## 1.0 UTANGULIZI

Mtihani wa somo la Uraia kwa Watahiniwa wa Ualimu ngazi ya Cheti (Daraja la A) ulifanyika mwezi Mei, 2023 na uliandaliwa kwa kuzingatia muhtasari wa somo la Uraia wa Mwaka 2009 na fomati ya mwaka 2022. Mtihani ulikuwa na maswali kumi na nne (14) ambapo mtahiniwa alitakiwa kujibu maswali yote kutoka sehemu A na B. Sehemu A ilikuwa na maswali kumi (10) ya majibu mafupi yenye jumla ya alama 40, kila swali likiwa na alama nne (4). Sehemu B ilikuwa na maswali manne (4) ya insha yenye jumla ya alama 60 ambapo kila swali likiwa na alama 15.

Ufaulu wa watahiniwa umegawanywa katika viwango vitatu ambavyo ni 'vizuri', 'wastani' na 'hafifu'. Ufaulu mzuri unaanzia alama 70 hadi 100, wastani alama 40 hadi 69, na hafifu alama 0 hadi 39. Aidha, chati za viwango vya ufaulu zimeambatishwa ili kufafanua ufaulu kwa watahiniwa ambapo rangi ya kijani inawakilisha ufaulu mzuri, njano ufaulu wa wastani na nyekundu inawakilisha ufaulu hafifu.

Takwimu zinaonesha kuwa somo hili lilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu. Kati ya watahiniwa 5,822 (100%) waliofanya mtihani, watahiniwa 5,753 (99.97%) walifaulu kwa kupata wastani wa alama 40 au zaidi na watahiniwa 89 (0.03 %) hawakufaulu. Ufaulu wa watahiniwa wa mwaka 2023 umeongezeka kwa asilimia 0.06 ikilinganishwa na ufaulu wa mwaka 2022, ambapo asilimia 99.81 ya watahiniwa waliofanya mtihani walifaulu.

Taarifa hii inachambua namna maswali yalivyojibiwa ili kupima kiwango cha ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Uraia. Uchambuzi huu unalenga kubaini umahiri wa watahiniwa katika kujibu maswali ya mtihani wa somo la Uraia. Sampuli za majibu yao zimeambatishwa ili kuonesha kilichotarajiwa kufanywa na kilichofanywa na watahiniwa. Aidha, taarifa inaonesha pia sababu zilizowafanya watahiniwa wachache kutopata alama za juu katika majibu ya maswali kwa baadhi ya mada. Hivyo, uchambuzi huu utasaidia kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Uraia ili kuboresha ufaulu wa watahiniwa katika mitihani ijayo.

## 2.0 UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WATAHINIWA KWA KILA SWALI

### 2.1 SEHEMU A: MASWALI YA MAJIBU MAFUPI

Sehemu hii ilikuwa na maswali 10 ambapo kila swali lilikuwa na jumla ya alama 4. Ufaulu wa watahiniwa uligawanywa katika makundi matatu, ambapo mtahiniwa alikuwa na ufaulu hafifu endapo alipata alama 0 hadi 1.5. Aidha, mtahiniwa alifaulu kwa wastani endapo alipata alama 2 hadi 2.5 na ufaulu ulikuwa mzuri endapo mtahiniwa alipata alama 3 hadi 4.

#### 2.1.1 Swali la 1: Dola

Swali lilimtaka mtahiniwa kutaja sifa nne za kujiunga na Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Jumla ya watahiniwa 5,822 (100%) walijibu swali hili, ambapo watahiniwa 3,205 (55%) walipata alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 2,255 (38.8%) walipata alama 2 hadi 2.5, na watahiniwa 362 (6.2%) walipata alama 3 hadi 4. Kwa ujumla ufaulu katika swali hili ulikuwa wa wastani kwa kuwa watahiniwa 2,617 (45%) walipata alama 2 hadi 4. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 1.




**Chati Na. 1:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 1*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa baadhi ya watahiniwa 3,205 (55%) waliopata alama 0 hadi 1.5 walidhihirisha kuwa na maarifa hafifu juu ya sifa za kujiunga na Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Mathalani, mtahiniwa mmoja alijibu hoja zisizo sahihi kama vile *awe ameukana uraia wa nchi yake,*

*ajiandikishe jina katika ofisi za uhamiaji, awe ana umri kuanzia miaka 18,* na *asiwe na kosa au kesi ya jinai huko katika nchi yake aliyoacha*. Aidha, mtahiniwa mwingine alitoa hoja zisizo sahihi ambazo ni *kutozijua sheria za nchi, kukosa uzalendo, kukosa kujua wajibu wake wa msingi,* na *kutokuwa na ushirikiano katika shughuli mbalimbali za nchi.* Majibu hayo ya watahiniwa yanaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha. Watahiniwa waliopata alama 0 hawakuwa na maarifa juu ya sifa za kujiunga na Jeshi la Wananchi wa Tanzania na walishindwa kuelewa matakwa ya swali, hivyo kutoa hoja zisizo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitaja sifa zisizo sahihi kama vile *sio Mtanzania, hajui sheria na kanuni za nchi ya Tanzania,* na *hajui katiba ya nchi*. Mtahiniwa mwingine aliandika hoja zisizo sahihi kama vile *hakutimiza miaka 18, hakuishi miaka mitano Tanzania, hakuwa na tabia njema,* na *aliwahi kufanya makosa.* Kielelezo Na. 1.1 ni sampuli ya jibu lisilo sahihi la mtahiniwa katika swali hili.


(a) Awe na akili timamu

(b) Aweze au afahamu lugha ya kiswahili na kiingereza kwa ufasaha.

(c) Awe na umri kuanzia miaka kumi na nane (18) na kuendelea.

(d) Awe ameishi Tanzania kwa takribani miezi kumi na mbili na zaidi au miaka ~~mika~~ mitano. (5)

**Kielelezo Na. 1.1:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 1.

Katika Kielelezo Na. 1.1, mtahiniwa alitaja sifa zinazotakiwa kwa Mtanzania kuajiriwa kufanya kazi badala ya sifa za kujiunga na Jeshi la Wananchi wa Tanzania.

Aidha, watahiniwa 2,255 (38.8%) waliopata alama 2 hadi 2.5 walikuwa na dosari mbalimbali katika majibu yao kama vile kuchanganya hoja sahihi na zisizo sahihi na wengine walitoa hoja pungufu au maelezo dhaifu na hivyo kushindwa kupata alama za juu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja, pamoja na kutoa hoja mbili sahihi aliandika pia hoja zisizo sahihi ambazo ni: *hakuwa na vyeti vya kuhitimu elimu ya sekondari* na *hakuwa na kadi ya mpiga kura*. Mtahiniwa mwingine aliandika hoja kama vile *alikosa sifa ya kuwa raia wa Tanzania, hakuwa na vitambulisho vinavyomtambulisha kuwa si Mtanzania, hakuwa mzalendo,* na *hakuwa na sifa za kujiunga kwa sababu ni raia wa nchi nyingine*. Katika hoja zilizotolewa na mtahiniwa huyu, hoja ya kwanza na ya tatu zilikuwa sahihi. Aidha, hoja ya pili na ya nne hazikuwa sahihi. Majibu hayo ya watahiniwa yanaonesha hawakuwa na

maarifa ya kutosha kuhusiana na sifa za kujiunga na Jeshi la Wananchi wa Tanzania.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 362 (6.2%) waliopata alama 3 hadi 4 walibainisha kwa usahihi sifa nne za kujiunga na Jeshi la Wananchi wa Tanzania. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya *Dola* na hasa mada ndogo ya *Uraia* na walielewa vema matakwa ya swali. Mfano wa majibu sahihi yaliyotolewa ni kama vile *awe mzaliwa wa Tanzania pamoja na wazazi wake, babu na bibi yake, awe mzalendo kwa nchi yake, awe ameandikishwa kuwa raia wa Tanzania,* na *awe anaipenda nchi yake.* Kielelezo Na. 1.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.


1 (i) Kutokua na uraia wa Tanzania kuliperekea asiaminiwe.
(ii) Kutokana na kutoukana uraia wa nchi yake.
(iii) Kutozaliwa Tanzania kulipelekea asiaminiwe.
(iv) Kutoonesha uzalendo wa nchi ya Tanzania.

**Kielelezo Na. 1.2:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 1.

### 2.1.2 Swali la 2: Dola

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kuainisha kazi nne za Bunge katika kutekeleza majukumu yake. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 5,822 (100%). Kati ya watahiniwa waliofanya swali hili, watahiniwa 338 (5.8%) walipata alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 1,005 (17.3%) walipata alama 2 hadi 2.5, na watahiniwa 4,479 (76.9%) walipata alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa watahiniwa 5,484 (94.2%) walipata alama 2 hadi 4. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 2.




**Chati Na. 2**: *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 2*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 4,479 (76.9%) waliopata alama 3 hadi 4 waliainisha kwa usahihi kazi nne za Bunge katika kutekeleza majukumu yake. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ndogo ya *Bunge na Baraza la Wawakilishi Zanzibar* kwa kuandika kwa usahihi hoja nne ambazo ni: *kutunga sheria, kusimamia serikali, kuwakilisha watu katika maamuzi ya kitaifa, kupitisha au kuidhinisha vyanzo vya mapato na matumizi ya serikali, kupitia na kuridhia mikataba ya kimataifa, kuthibitisha uteuzi wa Waziri Mkuu, kumchagua Spika wa Bunge, kuchunguza mikataba na Rushwa,* na *kupiga kura ya kutokuwa na imani na serikali*. Kielelezo Na. 2.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.


2
i. Bunge husaidia kuchagua spika na naibu spika
ii. Ni chombo cha kutunga sheria
iii. Kupokea, kujadili na kupitisha miswada mbali mbali
iv. Husaidia kumuondoa raisi aliyeko madarakani kwa kupiga kura ya kutokuwa na imani naye.

**Kielelezo Na. 2.1:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 2.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa watahiniwa 1,005 (17.3%) waliopata alama 2 hadi 2.5 wapo waliochanganya hoja sahihi na zisizo sahihi na wengine waliandika hoja pungufu. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja, pamoja na kutaja hoja mbili sahihi, pia alitaja hoja mbili zisizo sahihi ambazo ni kazi za Mahakama kama ifuatavyo: *kutafsiri sheria* na *kusimamia ulipwaji wa fidia*. Mtahiniwa mwingine alitoa hoja zifuatazo: *kutunga sheria, kukusanya mapato, kupitisha bajeti ya serikali* na

*kutatua migogoro mbalimbali ya wananchi.* Katika majibu ya mtahiniwa hoja ya kwanza na ya tatu zilikuwa sahihi wakati hoja ya pili na ya nne hazikuwa sahihi. Majibu hayo ya watahiniwa yanaonesha hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusiana na kazi za Bunge.

Aidha, kati ya watahiniwa 338 (5.8%) waliopata alama 0 hadi 1.5 baadhi yao walieleza kazi moja ya Bunge na wengine walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama vile *kutoa huduma za jamii, kutunga sheria za nchi, kusimamia haki za binadamu za msingi,* na *kusimamia ujenzi wa miundo mbinu*. Katika majibu yaliyotolewa na mtahiniwa huyu hoja ya pili tu ndiyo ilikuwa sahihi. Vilevile, watahiniwa waliopata alama 0 walidhihirisha kutokuwa na maarifa kuhusu kazi za Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kushindwa kutoa hoja sahihi na hawakuelewa vema matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja zisizo sahihi kama vile *usaidia kutetea haki za binadamu, usaidia kutatua migogoro ya wananchi, usaidia kuendeleza miundombinu,* na *usaidia kudumisha ulinzi na usalama.* Pia, mtahiniwa mwingine aliandika hoja zisizo sahihi ambazo ni *kutafsiri sheria, kugawanya madaraka kwa kila mbunge,* na *kumuapisha kiongozi wa nch*i. Kielelezo Na. 2.2 ni sampuli ya jibu lisilo sahihi la mtahiniwa katika swali hili.


2
i) Kulinda haki za binadamu
ii) Kutoa ajira
iii) Kuimalisha ulinzi na usalama
iv) Kulinda rasilimali za nchi

**Kielelezo Na. 2.2:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 2.

Katika Kielelezo Na. 2.2, mtahiniwa aliandika baadhi ya kazi za mhimili wa serikali badala ya kuainisha kazi nne za mhimili wa Bunge katika kutekeleza majukumu yake.

### 2.1.3 Swali la 3: Utamaduni Wetu

Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha mambo manne yanayoweza kumtofautisha raia wa kigeni na Mtanzania. Watahiniwa waliofanya swali hili walikuwa 5,822 (100%) ambapo watahiniwa 4,755 (81.7%) walipata alama 3 hadi 4, wataniniwa 822 (14.1%) walipata alama 2 hadi 2.5, na watahiniwa 245 (4.2%) walipata alama 0 hadi 1.5. Kwa ujumla, ufaulu wa watahiniwa katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa watahiniwa 5,577 (95.8%) walipata alama 2 hadi 4. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 3.




**Chati Na. 3:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 3*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 4,755 (81.7%) waliopata alama 3 hadi 4 walibainisha kwa usahihi mambo manne yanayoweza kumtofautisha raia wa kigeni na Mtanzania. Baadhi ya hoja sahihi zilizoandikwa ni kama vile *lugha, mavazi, mila na desturi,* na *vyakula*. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha juu ya kumtofautisha raia wa kigeni na Mtanzania na pia walielewa matakwa ya swali kama inavyoonekana kwenye sampuli ya jibu la mtahiniwa kwenye Kielelezo Na. 3.1.


3 (a) Lugha, watu wa jamii moja huwasiliana kwa lug
ha ya jamii yao mfano Tanzania kiswahili na kenya wan
atumia kingereza.
(b) Mavazi:- Mavazi ya watu wa tanzania ni tofauti na
watu wa kenya mf. Tanzania wana vaa khanga na madera
lakini kenya wanapendelea suti, suruali n.k.
(c) mila na desturi; Watu wa jamii tofauti hutofautiana
mila na desturi zao mfano namna ya kusalimiana, n.k.
(d) Vyakula.- Kutokana na utofauti wa nchi kasi na-
vyakula hutofautiana mf. Watu wa Tanzania chakula
la chao cha asilia ni Ugali (wa muhogo, mahindi).

**Kielelezo Na. 3.1:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 3.

Katika kundi la watahiniwa waliopata alama za wastani, watahiniwa wote 822 (14.1%) walipata alama 2. Watahiniwa hao walitoa hoja pungufu, wengine walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi na baadhi yao walirudia hoja sahihi mara mbili. Kwa mfano, jibu la mtahiniwa mmojawapo lilikuwa: *mila, uraia, mila*

na *lugha.* Katika majibu yaliyotolewa na mtahiniwa huyu, hoja ya mila na lugha zilikuwa sahihi wakati ambapo hoja ya uraia haikuwa sahihi na hoja ya mila ilijirudia. Mtahiniwa mwingine alijibu: *mila, desturi, lugha* na *maadili.* Katika majibu yaliyotolewa na mtahiniwa huyu, hoja ya mila na lugha zilikuwa sahihi wakati desturi na maadili zilijirudia. Majibu hayo ya watahiniwa yanaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusiana na mambo yanayoweza kumtofautisha raia wa kigeni na Mtanzania.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 245 (4.2%) wenye ufaulu hafifu walipata alama 0 hadi 1. Baadhi yao walitaja hoja pungufu ya mbili na wengine walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama vile l*ugha, ukabila, kibali/kitambulisho cha kuhamia nchi nyingine*, na *siasa*. Katika majibu ya mtahiniwa huyu, hoja ya kwanza tu ndiyo ilikuwa sahihi. Watahiniwa waliopata alama 0 hawakuwa na maarifa hivyo, kushindwa kubainisha kwa usahihi tofauti ya raia wa kigeni na Mtanzania japo kwa hoja moja. Baadhi yao walitofautisha mambo anayoyafanya Mtanzania na raia wa nchi nyingine. Baadhi yao walitofautisha majukumu ya kibayolojia kati ya mwanamke (Amina) na mwanaume (Katonge) waliotajwa kwenye swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa majibu yasiyo sahihi kama vile *Amina ana matiti na Katonge hana matiti, Amina anabeba mimba na Katonge habebi mimba,* na *Amina ananyonyesha na Katonge hanyonyeshi.* Mtahiniwa mwingine alitoa majibu kama vile *uraia, ukabila, mila na desturi,* na *utaifa.* Kielelezo Na. 3.2 ni sampuli ya jibu lisilo sahihi la mtahiniwa katika swali hili.



| 3 | Tanzania | Kenya |
|---|---|---|
| (i) | Raisi huchaguliwa iwapo akipita mpinzani wake hawezi kuwa Makamu wa raisi | Raisi anapochaguliwa mpinzani wake huwa Makamu. |
| (ii) | Mkoa husimamiwa na Mkuu wa Mkoa | Mkoa husimamiwa na gavana |
| (iii) | Elimu ya msingi ni darasa la 1 — 7 | Elimu ya msingi ni darasa la 1 — 8 |
| (iv) | Ni muungano wa Tanganyika na zanzibar (nchi mbili) | Si nchi ya Muungano. |

**Kielelezo Na. 3.2:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 3.

Katika Kielelezo Na. 3.2, mtahiniwa alibainisha upatikanaji wa viongozi katika ngazi mbalimbali badala ya kubainisha mambo manne yanayoweza kumtofautisha raia wa kigeni na Mtanzania.

### 2.1.4 Swali la 4: Uchumi wa Tanzania

Swali lilimtaka mtahiniwa kubainisha changamoto nne zinazowakabili wakulima katika shughuli zao. Swali lilijibiwa na watahiniwa 5,822 (100%) ambapo watahiniwa 447 (7.7%) walipata alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 1,359 (23.3%) walipata alama 2 hadi 2.5, na watahiniwa 4,016 (69%) walipata alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kuwa watahiniwa 5,375 (92.3%) walipata alama 2 hadi 4. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 4.




**Chati Na. 4:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 4*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 4,016 (69%) waliopata alama 3 hadi 4 walibainisha kwa usahihi changamoto nne zinazowakabili wakulima katika shughuli za kilimo. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ndogo ya *Nyanja za Uchumi*. Baadhi ya hoja sahihi zilizotolewa ni kama vile *ukosefu wa mitaji ya kutosha, ukosefu wa masoko, ukosefu wa elimu,* na *miundo mbinu mibovu.* Kielelezo Na. 4.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.



| 4 | |
|---|---|
| | (i) Kutokuwepo kwa Masoko endelevu yatakayowawezesha kuuza Mazao yao |
| | (ii) Gharama kubwa ya usafirishaji pale wanapopata soko Gharama inakuwa ni kubwa hivyo kutopata faida inayostahiki |
| | (iii) Kutokuwa na elimu ya kutosha kuhusiana namna nzuri ya kuzalisha Mazao hayo ili iwawezesha kuwapata faida. |
| | (iv) Uhaba wa pembejeo za kilimo hiyo pia ni changamoto kwani hupelekea kupata Mazao kiasi chache. |

**Kielelezo Na. 4.1:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 4.

Kwa upande mwingine, katika kundi la watahiniwa wenye ufaulu wa wastani, watahiniwa wote 1,359 (23.3%) walipata alama 2 kutokana na hoja zao kuwa na mapungufu mbalimbali. Baadhi yao waliainisha changamoto pungufu na wengine walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi. Kwa mfano mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama vile *kukosekana kwa miundo mbinu bora, ukosefu wa masoko na viwanda kwa ajiri ya biashara, ukosefu wa ajira za kutosha katika ngazi ya uchumi,* na *ukosefu wa rasilimali za taifa*. Katika majibu ya mtahiniwa, hoja ya kwanza na ya pili zilikuwa sahihi wakati hoja ya tatu na ya nne hazikuwa sahihi. Mtahiniwa mwingine alijibu kwa kutoa hoja ambazo ni: *ukosefu wa mbegu bora, kutolima kwa kutumia mistari, kuchanganya mazao ya biashara na ya chakula,* na *ukosefu wa ushauri wa wataalamu mbalimbali wa kilimo*. Katika majibu ya mtahiniwa, hoja ya kwanza na ya nne zilikuwa sahihi wakati hoja ya pili na ya tatu hazikuwa sahihi. Majibu hayo ya watahiniwa yanaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusiana na changamoto zinazowakabili wakulima katika shughuli zao.

Watahiniwa 447 (7.7%) wenye ufaulu hafifu walipata alama 0 hadi 1 kutokana na kushindwa kuainisha changamoto zinazowakabili wakulima. Baadhi yao waliaininsha kwa usahihi changamoto moja au walichanganya hoja moja sahihi na zingine zisizo sahihi. Hii ina maana kuwa watahiniwa hao hawakuelewa vema matakwa ya swali na hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya nyanja za uchumi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika hoja kama vile *sera mbaya ya nchi, mirundikano ya bidhaa nyingi kutoka nje ya nchi, bei kuwa chini ya kiwango,* na *bidhaa zinazozalishwa kutokuwa na ubora wa kukidhi viwango vya wahitaji*. Katika majibu ya mtahiniwa huyu, hoja ya tatu ndiyo ilikuwa sahihi. Watahiniwa ambao walipata alama 0 hawakuwa na maarifa kabisa hivyo walishindwa kulielewa swali. Baadhi yao hawakufanya swali hilo na wengi wao walishindwa kuainisha kwa usahihi hoja hata moja. Kwa mfano, mtahiniwa mmojawapo alitoa

hoja zisizo sahihi kama vile *kuwepo kwa aridhi isiyo na rutuba, ufugaji wa holela ambao huathiri aridhi na kuchoka, kilimo cha kisasa katika mashamba makubwa,* na *mwingiliano wa mazao mbalimbali katika eneo moja*. Mtahiniwa mwingine alitoa hoja zisizo sahihi kama vile *kushindwa kubaini zao la chakula linalopendwa sana na watu, watu wengi kulima zao la aina moja, kupuuzia biashara zao na kutothamini ubora wa mazao,* na *mazao mengi huhifadhiwa kwa muda mrefu*. Kielelezo Na. 4.2 ni sampuli ya jibu lisilo sahihi la mtahiniwa katika swali hili.



| 4 | i) Uchimbaji madini |
|---|---|
| | ii) shughuli za viwanda |
| | iii) mmomonyoko wa ardhi |
| | iv). Ukataji wa miti ovyo |

**Kielelezo Na. 4.2:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 4.

Katika Kielelezo Na. 4.2, mtahiniwa alieleza juu ya dhana za uzalishaji mali na athari za shughuli za binadamu badala ya kuainisha changamoto nne zinazowakabili wakulima katika shughuli za kilimo.

### 2.1.5 Swali la 5: Uchumi wa Tanzania

Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa ufupi hoja nne juu ya faida za utandawazi kiuchumi. Swali hili lilijibiwa na watahiniwa 5,822 (100%) ambapo watahiniwa 569 (9.8%) walipata alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 1,701 (29.2%) walipata alama 2 hadi 2.5, na watahiniwa 3,552 (61%) walipata alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, ufaulu katika swali hili ulikuwa mzuri kwa kuwa watahiniwa 5,253 (90.2%) walipata alama 2 hadi 4. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 5.




**Chati Na. 5:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 5*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 3,552 (61%) waliopata alama 3 hadi 4 walieleza kwa usahihi faida za utandawazi kiuchumi. Baadhi ya majibu sahihi yaliyoandikwa na watahiniwa ni kama vile *kukua kwa uchumi wa soko huria, kukua kwa njia za uchukuzi na mawasiliano, kukua kwa teknolojia,* na *kuboreshwa kwa miundo mbinu*. Watahiniwa hao walionesha kuwa na maarifa ya kutosha katika mada ndogo ya *Mambo yanayochangia kukua au kuporomoka kwa uchumi*. Vilevile, watahiniwa walielewa vema matakwa ya swali. Kielelezo Na. 5.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.


5

mchango wa utandawazi uchumi Tanzania.
i) kukua kwa uchumi wa soko huria.
mfano Raia wa kenya anaweza kuleta bidhaa
yake nchini na watanzania pia pasipo kizuizi.

ii) kukua kwa njia za uchukuzi na mawasiliano.
kila mtanzania anaweza kutumia simu kuagi-
za mzigo wake kutoka mahali popote nchini na
mikoani.
iii) kukua kwa sayansi na teknolojia.
mfano unaweza kutumia mwamala kutuma pesa.
badala ya kutumia posta.
iv) kuboresha kwa miundombinu. mfano -
katika usafiri, masoko na bandari.

**Kielelezo Na. 5.1:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 5.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 1,701 (29.2%) waliopata alama 2 hadi 2.5 walitoa hoja zenye mapungufu mbalimbali kama vile kutoa hoja pungufu na kuchanganya hoja sahihi na zisizo sahihi. Wengine waliandika hoja dhaifu ambazo kila hoja ilipewa nusu ya jumla ya alama hivyo kupata alama za wastani. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alichanganya hoja mbili zisizo sahihi katika majibu yake ambazo ni *hifadhi za mazingira na elimu* na *husaidia kuleta amani na utulivu.* Majibu hayo ya watahiniwa yanaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya faida za utandawazi kiuchumi.

Uchambuzi zaidi unaonesha kuwa baadhi ya watahiniwa 569 (9.8%) waliopata alama 0 hadi 1.5 walikuwa na maarifa hafifu kuhusu faida nne za utandawazi

kiuchumi hivyo walichanganya hoja moja sahihi na zingine zisizo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alijibu kuwa: *kuboresha huduma za jamii, kuboresha miundo mbinu, kuboresha huduma za jamii,* na *ushirikiano kwa watu*. Katika majibu ya mtahiniwa huyu, hoja ya pili ndio ilikuwa sahihi. Watahiniwa waliopata alama 0 hawakuwa na maarifa kuhusu dhana iliyoulizwa. Baadhi yao hawakuelewa matakwa ya swali, hivyo kutoa hoja zisizo sahihi. Kwa mfano mtahiniwa mmoja alitoa hoja kwamba: *hutusaidia kupata wataalamu, hutusaidia kupata misaada,* na *hutusaidia katika biashara unaweza kununua ndani na nje ya nchi*. Mtahiniwa mwingine aliandika hoja kama vile *uboreshaji wa viwanda* na *nguvu kazi ya taifa kupanda* ambayo si majibu sahihi. Kielelezo Na. 5.2 ni sampuli ya jibu lisilo sahihi la mtahiniwa katika swali hili.


5
(i) mmomonyoko wa maadili hii inatokana na utandawazi mfano kwa asilimia sitini vijana wengi wanatumia simu janja ambazo ni mambo mengi ya hovyo kama kuangalia picha au video za ngono.
(ii) Kuharibika kwa mila na desturi za watanzania na kuiga za kigeni. mfano tamaduni kula kwa vijiko hii ni ya kuiga.
(iii) Kukua kuongezeka kwa wizi wa kidigitali zaidi, kutokana kuwepo ~~mitandao~~ mitandao wa kijamii watu wanaibiwa kwa njia ya mtandaoni
(iv) magonjwa. mfano magonjwa ya macho hii inatokana na utumiaji sana wa simu au kompyuta kwa muda mrefu.

**Kielelezo Na. 5.2**: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 5.

Katika Kielelezo Na. 5.2, mtahiniwa alieleza athari nne za utandawazi kijamii badala ya kueleza faida nne za utandawazi kiuchumi.

### 2.1.6 Swali la 6: Misingi ya Ufundishaji wa Somo la Uraia.

Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa ufupi tofauti nne zilizopo kati ya stadi ya mawasiliano aliyonayo Sakala na stadi ya udadisi na ubunifu aliyonayo Muli. Kati ya watahiniwa 5,822 (100%) waliofanya swali hili, watahiniwa 4,324 (74.3%) walipata alama 3 hadi 4, watahiniwa 748 (12.8 %) walipata alama 2 hadi 2.5, na

watahiniwa 750 (12.9 %) walipata alama 0 hadi 1.5. Kwa ujumla swali hili lilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kuwa watahiniwa 5,072 (87.1%) walipata alama 2 hadi 4. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 6.




**Chati Na. 6:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 6*

Uchambuzi wa ufaulu katika swali hili unaonesha kuwa watahiniwa 4,324 (74.3%) waliopata alama 3 hadi 4 walikidhi matakwa ya swali kwa kueleza kwa usahihi tofauti nne kati ya Sakala na Muli kwa kuzingatia stadi zao. Baadhi ya majibu sahihi yaliyotolewa na watahiniwa hao ni *Sakala ana stadi ya kuwasiliana lakini Muli ana ujuzi wa kudadisi, Sakala ana uwezo wa kutumia mitindo mbalimbali katika kupashana habari wakati Muli ana stadi ya kuunda, kufikiri na kudodosa vitu mbalimbali, Sakala huangalia ubora katika kupashana habari lakini Muli hufanya uchunguzi yakinifu na kudodosa taarifa mbalimbali,* na *Sakala hujikita katika ujuzi wa kutumia lugha wakati Muli hutumia lugha katik*a *udadisi*. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ndogo ya *Ufundishaji unaozingatia ujenzi wa stadi na ujuzi wa kiraia*. Kielelezo Na. 6.1 ni sampuli ya jibu sahihi la mtahiniwa katika swali hili.


6

(i) Sakala ana stadi ya kuwasiliana kwa kutumia lugha kwa namna tofauti LAKINI Muli ana ujuzi wa kudadisi na ~~kubuni~~ ubunifu wa vitu mbalimbali

(ii) Sakala ana ujuzi wa kutumia mtindo mbalimbali katika njeo, viambishi vya lugha LAKINI, muli ana stadi mbali ya kuunda, kufikiri, na kudadisi vitu mbalimbali

(iii) Stadi ya Sakala huangalia ubora katika kupashana habari, ~~na~~ kwa namna tofauti na kupata taarifa LAKINI stadi ya muli huangalia hali nzima katika kufanya uchunguzi yakinifu na kudadisi taarifa mbalimbali

(iv) Stadi ya Sakala hujikita katika ujuzi wa kutumia lugha LAKINI Stadi ya muli haitumii lugha maana hujikita ktk utendaji wa udadisi na kubuni

**Kielelezo Na. 6.1:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 6.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 750 (12.9%) waliopata alama 0 hadi 1 walikuwa na maarifa hafifu kwa kuwa walieleza kwa usahihi hoja moja na wengine walichanganya hoja moja sahihi na zingine zisizo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja moja sahihi ambayo ni *Sakala inahusika na masuala ya mawasiliano wakati Muli inahusika na masuala ya udadisi na ubunifu tu*. Mtahiniwa mwingine alitoa hoja kama vile *Sakala hutumia lugha katika mawasiliano wakati Muli hutumia sanaa za picha na michoro, Sakala hutumia intaneti wakati Muli haitumii intaneti,* na *Sakala huburudisha jamii kutoka sehemu tofauti tofauti wakati Muli hufurahisha jamii kutoka eneo alilopo mbunifu*. Katika majibu ya mtahiniwa hoja ya kwanza tu ndio ilikuwa sahihi. Watahiniwa waliopata alama 0, hawakuelewa matakwa ya swali hivyo walitoa hoja zisizo sahihi. Aidha, watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutofautisha dhana ya Sakala na Muli. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja zisizo sahihi kama vile *maarifa mbalimbali kujumuisha redio, simu, na magazeti huelimisha jamii,* na *uzalendo*. Pia, mtahiniwa mwingine alitoa hoja kama vile *Sakala anajihusisha na sayansi na teknolojia wakati Muli anajihusisha na uchukuzi na utafiti, Sakala anajishughulisha na ukuaji wa utandawazi lakini Muli anajihusisha na ujuzi na maarifa,* na *Sakala anahusika na kupatikana kwa habari wakati Muli anajihusha na ubunifu wa vitu mbalimbali*. Kielelezo Na. 6.2 ni sampuli ya jibu lisilo sahihi la mtahiniwa katika swali hili.


6

(i) Maarifa Mbali Mbali

(ii) Hujumuisha Redio Simu na Magazeti

(iii) Huelimisha Jamii

(iv) Uzalendo

**Kielelezo Na. 6.2:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 6.

Katika Kielelezo Na. 6.2, mtahiniwa aliainisha dhana mbalimbali zisizo sahihi kwa kuziorodhesha badala ya kubainisha tofauti kati ya Sakala na Muli.

Pia, uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 748 (12.8%) walipata ufaulu wa wastani wa alama 2. Baadhi yao walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi na wengine kutaja hoja pungufu ya tatu kinyume na matakwa ya swali. Mtahiniwa mmoja alitoa hoja kama vile *Sakala hutumia lugha katika kufanya mawasiliano lakini Muli hutumia sanaa za picha na michoro ili kufanya udadisi, Sakala hutumia intaneti wakati Muli hatumii intanet kwa matumizi,* na *Sakala huburudisha jamii kutoka sehemu tofauti tofauti lakini Muli hufurahisha jamii kutokana na eneo alilopo mbunifu na mdadisi.* Katika majibu ya mtahiniwa huyu, hoja ya kwanza na ya tatu zilikuwa sahihi wakati hoja ya pili haikuwa sahihi. Majibu hayo ya watahiniwa yanaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha hususan katika mada ndogo ya *ufundishaji unaozingatia ujenzi wa stadi na ujuzi wa kiraia*.

### 2.1.7 Swali la 7: Utamaduni Wetu

Swali lilimtaka mtahiniwa kutaja mila nne zinazoweza kusababisha maambukizi ya UKIMWI. Watahiniwa 5,822 (100%) walijibu swali hili ambapo watahiniwa 57 (1%) walipata alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 156 (2.7%) walipata alama 2 hadi 2.5, na watahiniwa 5,609 (96.3%) walipata alama 3 hadi 4. Kwa ujumla swali hili lilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kuwa watahiniwa 5,765 (99%) walipata alama 2 hadi 4. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 7.




**Chati Na. 7:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 7*

Uchambuzi wa ufaulu katika swali hili unaonesha kuwa watahiniwa 5,609 (96.3%) waliopata alama 3 hadi 4 walikidhi matakwa ya swali kwa kutaja kwa usahihi mila nne zinazoweza kusababisha maambukizi ya UKIMWI ambazo ni *ukeketaji, ndoa za utotoni, kuoa wanawake wengi,* na *kurithi wajane*. Majibu mengine sahihi yaliyotolewa ni kama vile *tohara kwa wanawake, ndoa za mitala na kutakasa wajane*, na *ndoa za kulazimisha*. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mila zinazoweza kusababisha maambukizi ya UKIMWI. Kielelezo Na. 7.1 ni sampuli ya jibu sahihi la mtahiniwa katika swali la 7.


i Kurithi wajane, hiki ni kitendo cha ~~mume~~ mke au mume
aliyefiwa na mume au mke kuolewa na mtu mwingine
hivyo huweza kuchangia maambukizi ya ukimwi

ii Ukeketaji, hii ni mila na desturi nyingine ambayo huweza
kuchangia maambukizi ya ukimwi kwani ngariba hutumia
kifaa kimoja kukeketa watu zaidi ya mmoja

iii Ndoa za mitara, hiki ni kitendo cha kuoa mke zaidi ya mmoja
au kitendo cha mwanaume mmoja kuoa wake au mke zaidi
ya mmoja ambapo huchangia kuenea kwa maambukizi ya ukimwi

iv Ndoa za kulazimishwa, baadhi ya makabila huwa na mila
na desturi ya kuwalazimisha watoto wao kuoa au kuolewa na
watu asiyempenda na asiyemtaka yeye hivyo huchangia maambukizi

**Kielelezo Na. 7.1:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 7.

Aidha, watahiniwa 156 (2.7%) waliopata alama 2 baadhi yao walitoa hoja pungufu na wengine walichanganya mila na njia zinazoeneza maambukizi ya UKIMWI. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi katika majibu yake kwa kuandika *ukeketaji, tohara, kutoga masikio,* na *kufanya ngono zembe bila kinga*. Katika majibu ya mtahiniwa huyo, hoja ya kwanza na ya pili ni sahihi wakati hoja ya tatu na ya nne siyo sahihi kwa kuwa ni njia za kueneza UKIMWI. Majibu hayo yanaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mila zinazoweza kusababisha maambukizi ya UKIMWI.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 57 (1%) waliopata ufaulu hafifu walipata alama 0 hadi 1. Baadhi yao walitaja mila pungufu ya mbili na walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja moja tu ambayo ni *ukeketaji.* Mtahiniwa mwingine alitoa hoja kama vile *ukeketaji, ngono zembe, uchangiaji wa vifaa vyenye ncha, uasherati,* na *ubakaji.* Katika majibu ya mtahiniwa huyu, hoja ya kwanza tu ndiyo ilikuwa sahihi. Watahiniwa waliopata alama 0 walishindwa kutaja kwa usahihi hoja hata moja. Wengi waliainisha njia zinazosababisha kuenea kwa maambukizi ya UKIMWI badala ya mila ambazo zilikuwa takwa la swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika hoja zisizo sahihi kama vile *kuoa au kuolewa, kuchangia damu, ukosefu wa elimu,* na *imani potofu*. Mtahiniwa mwingine alitoa majibu kama vile *kuchangia vifaa vyenye ncha kali, kujamiana bila kinga au ngono zembe, kuhamishiwa damu isiyo salama,* na

*kunyonyesha kwa mama na mtoto*. Kielelezo Na. 7.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.




**Kielelezo Na. 7.2:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 7.

Katika Kielelezo Na. 7.2, mtahiniwa ametaja majina ya makabila mbalimbali badala ya mila zinazoweza kusababisha kuenea kwa maambukizi ya UKIMWI, hivyo kupata alama 0.

### 2.1.8 Swali la 8: Zana za Kufundishia na Kujifunzia

Swali lilimtaka mtahiniwa atumie mifano miwili kwa kila kundi kufafanua makundi mawili ya zana za kufundishia na kujifunzia. Watahiniwa 5,822 (100%) walijibu swali hili, ambapo watahiniwa 1,971 (33.9%) walipata alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 310 (5.3%) walipata alama 2 hadi 2.5, na watahiniwa 3,541 (60.8%) walipata alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu kwa kuwa watahiniwa 3,851 (66.1%) walipata alama 2 hadi 4. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 8.




**Chati Na. 8:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 8*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 3,541 (60.8%) waliopata alama 3 hadi 4 walitoa mifano sahihi miwili kwa kila kundi kufafanua makundi mawili ya zana za kufundishia na kujifunzia. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu Zana za Kufundishia na Kujifunzia hususani kwenye mada ndogo ya *Aina za Zana*. Baadhi ya hoja sahihi zilizotolewa ni kama vile *zana maono ambazo huhusisha macho katika kuona na kujifunzia kwa mfano picha na runinga* na *zana masikizi ambazo huhusisha masikio katika kusikia na kujifunzia kwa mfano redio na kanda mbalimbali.* Kielelezo Na. 8.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.


(a) Zana masikizi, ni aina ya zana ambazo hu
tumia mlango wa Fahamu wa masikio, Mwa
limu anaweza kutumia zana masikizi kama redi
o, tepu rekoda n.k. Zana hizi huvuta usiki
vu kwa wanafunzi
(b) Zana maono, ni aina ya zana za kufundishi
a na kujifunzia ambazo wanafunzi hujifunza
Kwa kuona mfano picha na michoro mbalimb
ali, Zana hizi huweza kumjengea mwanafunzi
Kumbukumbu ya Muda Mrefu kwa sababu anafu
Funza kwa kuona.

**Kielelezo Na. 8.1:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 8.

Kwa upande mwingine, baadhi ya watahiniwa 1,971 (33.9%) waliopata alama 0 hadi 1.5 hawakutoa mifano miwili au walichanganya makundi ya zana za kufundishia na kujifunzia na aina au njia za upatikanaji wa zana za kufundishia na kujifunzia. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja mbili bila maelezo wala mifano: *zana za masikizi* na *zana za maono.* Hoja zote mbili zilikuwa sahihi lakini zilikosa maelezo na mifano. Watahiniwa waliopata alama 0 hawakutoa mifano miwili katika kufafanua makundi mawili ya zana za kufundishia na kujifunzia. Walidhihirisha kuwa hawana maarifa juu ya makundi mawili ya zana za kufundishia na kujifunzia. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: *zana za kisasa za kufundishia na kujifunzia kwa mfano video na projekta, zana mafunzo za kufundishia na kujifunzia kwa mfano ubao na projekta,* na *zana mpitisho za kufundishia na kuijifunzia kwa mfano majarida na magazeti.* Mtahiniwa mwingine alitoa majibu yafuatayo: *zana za asili mfano matawi, mawe* na *zana za bandia au kisasa mfano chati*. Kielelezo Na. 8.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.



| | |
|---|---|
| (P) | Picha na michoro |
| | Mfano ngao ya taifa na bendera ya |
| | Tanzania. |
| (ii) | Vitu halisi |
| | Mfano ngoma na mavazi ya asili |

**Kielelezo Na. 8.2**: Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 8.

Katika Kielelezo Na. 8.2, mtahiniwa alitaja vitu/vifaa vyenye uhusiano wa karibu na zana za kufundishia na kujifunzia badala ya makundi ya zana za kufundishia na kujifunzia somo la Uraia.

Aidha, watahiniwa 310 (5.3%) walipata alama 2 hadi 2.5 kutokana na mapungufu mbalimbali katika majibu yao kama vile kuchanganya hoja sahihi na zisizo sahihi na baadhi yao maelezo hayakuwa na mifano. Hivyo, walipata alama za wastani. Watahiniwa wengine waliandika hoja dhaifu ambazo kila hoja ilipata nusu ya jumla ya alama. Baadhi ya majibu ya watahiniwa yalikuwa ni *zana za asili ambazo zinapatikana katika mazingira aliyeko mwalimu na mtoto kwa mfano picha za vitu, chati za michoro* na *zana za kisasa ambazo si rahisi kupatikana katika mazingira mfano runinga na kompyuta.* Katika majibu ya mtahiniwa, hoja zote zilikuwa dhaifu ambapo kila hoja ilipata nusu ya alama moja na jumla akapata alama 2. Majibu hayo yanaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mifano ya makundi ya zana za kufundishia na kujifunzia.

### 2.1.9 Swali la 9: Maandalizi ya Kufundisha Somo la Uraia

Swali lilimtaka mtahiniwa kutoa hoja nne kuthibitisha kuwa ili kuandaa azimio bora la kazi kwa somo la Uraia, mwalimu anapaswa kufanya uchambuzi wa muhtasari. Kati ya watahiniwa 5,822 (100%) waliojibu swali hili, watahiniwa 310 (5.3%) walipata alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 536 (9.2%) walipata alama 2 hadi 2.5, na watahiniwa 4,976 (85.5%) walipata alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kuwa watahiniwa 5,512 (94.7%) walipata alama 2 hadi 4. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 9.




**Chati Na. 9:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 9*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 4,976 (85.5%) waliopata alama 3 hadi 4 walithibitisha kwa usahihi kuwa ili mwalimu aweze kuandaa azimio bora la kazi kwa somo la Uraia anapaswa kufanya uchambuzi wa Muhtasari. Watahiniwa hao walithibitisha kwa kutoa hoja sahihi kama vile *kubaini mada zitakazofundishwa, kubaini mbinu za kufundishia na kujifunzia, kubaini zana za kufundishia na kujifunzia,* na *kubaini rejea zinazopaswa kutumika katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji*. Kielelezo Na. 9.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyetoa majibu sahihi katika swali hili.


9
i) Muhtasari humsaidia mwalimu katika upangiliaji wa mada zote kwa usahihi na mtiririko mzuri.
ii) Kwasababu muhtasari hupendekeza mbinu za ufundishaji na ujifunza.
iii) Kwasababu muhtasari huonyesha zana za kufundishia katika mada husika.
iv) Kwasababu muhtasari humsaidia mwalimu katika kubaini zana za upimaji atakazoweza zitumia.

**Kielelezo Na. 9.1:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 9.

Hata hivyo, watahiniwa 536 (9.2%) waliopata alama 2 hadi 2.5 walitaja hoja pungufu na wengine walirudia hoja zaidi ya mara moja. Aidha, katika kundi hili wapo waliochanganya hoja sahihi na zisizo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja zifuatazo: *humsaidia mwalimu kuandaa azimio la kazi, humsaidia mwalimu kuandaa andalio la somo,* na *humsaidia mwalimu kuandaa nukuu za somo.* Hoja hizo zilionesha kuwa mtahiniwa hakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu umuhimu wa kuchambua muhtasari kwa mwalimu ili kuandaa azimio bora la kazi kwa somo la Uraia.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 310 (5.3%) waliopata alama 0 hadi 1.5 walitoa hoja pungufu ya mbili au walichanganya hoja moja sahihi na zingine zisizo sahihi. Watahiniwa waliopata alama 0 walishindwa kuthibitisha kuwa ili kuandaa azimio bora la kazi kwa somo la Uraia, mwalimu anapaswa kufanya uchambuzi wa muhtasari. Watahinwa hao walidhihirisha kutokuwa na maarifa kuhusu dhana husika na hawakuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano mtahiniwa mmoja aliandika hoja zisizo sahihi ambazo ni: *mwalimu anapaswa kuwa na kalenda ya shule* na *kalenda ya mwaka mzima na mihula yote*. Mtahiniwa mwingine aliandika: *kuwa na kitabu cha kiada* na *ratiba za masomo na utungaji wa mitihani.* Kielelezo Na. 9.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu kwa usahihi swali hili.


9 Uchambuzi wa muhtasari katika kuandaa Azimio la kazi.
i> Kupanga mada rahisi kwenda ngumu.
ii> Kupanga mada kulingana na uhusiano
iii> kulingana na mazingira.
iv> kulingana na umri na uelewa wa wanafunzi.

**Kielelezo Na. 9.2:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 9.

Katika Kielelezo Na. 9.2, mtahiniwa aliainisha dhana na misingi mbalimbali inayotumika katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Uraia badala ya kuthibitisha umuhimu wa kuchambua muhtasari kwa mwalimu ili kuandaa azimio bora la kazi kwa somo la Uraia.

### 2.1.10 Swali la 10: Dola

Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza kwa ufupi aina nne za uraia katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kati ya watahiniwa 5,822 (100%) waliofanya swali hili, watahiniwa 285 (4.9%) walipata alama 0 hadi 1.5, watahiniwa 593 (10.2%) walipata alama 2 hadi 2.5, na watahiniwa 4,944 (84.9%) walipata alama 3 hadi 4. Kwa ujumla, kiwango cha ufaulu katika swali hili kilikuwa kizuri kwa kuwa watahiniwa 5,537 (95.1%) walipata alama 2 hadi 4. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 10.




**Chati Na. 10:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 10*

Uchambuzi wa ufaulu katika swali hili unaonesha kuwa watahiniwa 4,944 (84.9%) waliopata alama 3 hadi 4 walikuwa na maarifa ya kutosha katika mada ndogo ya *Uraia*. Watahiniwa hao waliweza kutoa hoja sahihi tatu hadi nne kuhusu aina ya uraia. Majibu sahihi yaliyotolewa yalikuwa: *uraia wa kuzaliwa; ambao mtu huzaliwa katika taifa husika na kuwa raia, uraia wa kuandikishwa; ambao mtu husajiliwa katika taifa kwa kufuata taratibu zote za msingi, uraia wa kuoa au kuolewa; ambapo mtu anaweza kuolewa katika taifa hili,* na *uraia wa kurithi, huu ni uraia ambao unapatikana kwa kurithi kwa wazazi.* Kielelezo Na. 10.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.


10
i) Uraia wa kuzaliwa, Huu ni aina ya uraia ambao mtu huzaliwa katika taifa husika na kuwa raia wa taifa hilo

ii) Uraia wa kuandikishwa. Ni aina ya uraia ambao mtu Uomba kuandikishwa katika taifa kwa kufuata taratibu zote za nchi

iii) Uraia wa kuoa au kuolewa. Hii ni aina ya uraia ambapo mtu anaruhusiwa kuoa au kuolewa katika taifa hilo

iv) Uraia wa kurithi, Uraia mwingine ambao mtu huweza kupata kwa kurithi kwa wazazi

**Kielelezo Na.** 10.1: Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 10.

Kwa upande mwingine, uchambuzi unaonesha kuwa watahiniwa 593 (10.2%) walipata alama 2 hadi 2.5 kwa sababu walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi. Aidha, baadhi yao walitoa hoja pungufu ya tatu na kushindwa kukidhi mahitaji ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alijibu: *uraia wa kuhamia ni aina ya uraia ambao mtu kutoka nchi nyingine mfano Uganda anahamia Tanzania moja kwa moja, uraia wa kupewa hutolewa na nchi au taifa fulani,* na *uraia wa asili/jadi*. Majibu hayo, yanaonesha kuwa watahiniwa katika kundi hili hawakuwa na maarifa ya kutosha juu ya aina za uraia katika Jamhuri ya Muungano Tanzania.

Aidha, baadhi ya watahiniwa 285 (4.9%) waliopata alama 0 hadi 1.5 walikuwa na maarifa hafifu juu ya aina za uraia. Waliandika hoja sahihi moja au hoja nyingine zilikuwa tofauti na mahitaji ya swali. Watahiniwa waliopata alama 0 hawakuwa na maarifa juu ya aina za uraia na hawakuweza kuelewa matakwa ya swali kwa sababu hawakuweza kuandika hoja sahihi hata moja. Kwa mfano mtahiniwa mmoja aliandika hoja zisizo sahihi ambazo ni: *uraia wa kisiasa, uraia wa maendeleo ya uchumi* na *uraia wa kuhamia*. Mtahiniwa mwingine aliandika hoja zisizo sahihi kama vile *uraia wa mzalendo; mfano kuwa mzalendo katika chama cha CCM, uraia wa mkazi; mfano mtu kuwa mkazi katika mkoa fulani Tanzania, uraia wa kuandikwa; mfano wakati wa sensa mtu kuhesabiwa sehemu aliyopo/anayoishi,* na *uraia wa uhusiano kati ya mtu na dola yake*. Kielelezo Na. 10.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kukidhi matakwa ya swali.


10

AINA ZA URAIA KATIKA JAMHURI YA MUUNGANO WA TZ.

i) Urafa wa Kiuchumi Mfano. kupata sehemu/maeneo ya Ardhi ya kulima mazao ya chakula na biashara, kuwa na sehemu ya kufanya biashara. na usoni.

ii) Urafa wa Kisiasa na kiraia Mfano, kutaka kutoa maoni, kuchagua na kuchaguliwa, kushiriki katika mikutano ya kisiasa na kupata elimu.

iii) Urafa wa Kijamii Mfano kupata makazi ya kuishi, huduma za afya mfano vidonge, sindano, huduma ya maji, shule.

iv) Urafa wa kimazingira na kimaendeleo Mfano kushiriki kufanya usafi wa mazingira, kutoa kodi.

**Kielelezo Na. 10.2:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 10.

Katika Kielelezo Na. 10.2, mtahiniwa aliainisha ushiriki wa raia katika nyanja za maisha kama vile uchumi, siasa, na kijamii badala ya aina za uraia katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

## 2.2 SEHEMU B: MASWALI YA INSHA

Katika sehemu hii, kila swali lilikuwa na jumla ya alama 15. Ufaulu wa watahiniwa uligawanywa katika makundi matatu. Mtahiniwa aliyepata alama 0 hadi 5.5 alikuwa na ufaulu hafifu, mtahiniwa aliyepata alama 6 hadi 10 alifaulu kwa wastani, na aliyepata alama 10.5 hadi 15 alikuwa na ufaulu mzuri.

### 2.2.1 Swali la 11: Uchambuzi wa Maandiko/Machapisho Muhimu ya Kufundishia /Kujifunzia Somo la Uraia

Swali hili lilimtaka mtahiniwa kueleza sifa kuu tano zitakazomwezesha mwalimu kuchagua machapisho bora katika muktadha wa somo la Uraia. Kati ya watahiniwa 5,822 (100%) waliofanya swali hili, watahiniwa 395 (6.8%) walipata alama 0 hadi 5.5, watahiniwa 1,645 (28.2%) walipata alama 6 hadi 10, na watahiniwa 3,782 (65%) walipata alama 10.5 hadi 15. Kwa ujumla swali hili lilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kuwa watahiniwa 5,427 (93.2%) walipata alama 6 hadi 15. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na.11.




**Chati Na. 11:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 11*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 3,782 (65%) waliopata alama 10.5 hadi 15 walikidhi matakwa ya swali kwa kueleza kwa usahihi sifa kuu tano zitakazomwezesha mwalimu kuchagua machapisho bora katika muktadha wa somo la Uraia. Wengi kati yao walianza na utangulizi uliojitosheleza, walikuwa na maelezo sahihi ya kutetea hoja zao na walikuwa na hitimisho linaloakisi hoja zilizotolewa. Baadhi ya hoja sahihi zilizoandikwa na watahiniwa hao ni *yawe na uhusiano na mada inayofundishwa katika darasa husika, yawe yameandikwa kwa lugha nyepesi na inayoeleweka, yawe yanapatikana kwa urahisi katika mazingira yao,* na *maudhui yake yawahamasishe wanafunzi kuwa wabunifu na kufikiri kwa kina*. Kielelezo Na. 11.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

11 Machapisho Ni jumla ya vitu vyote vilivyochapwa ambavyo hutumika ~~kwa~~ kuwapatia wanafunzi maarifa mapya katika ujifunzaji na ufundishaji mfano wa Machapisho ni pamoja na majarida, magazeti, vitabu mbalimbali - Machapisho ya kufundishia Somo la Uraia yanapaswa kuwa na Sifa mbalimbali hasa pale ~~watoto~~ wanapoyachagua Mwalimu anapotaka kuchagua.

Yapatikane katika mazingira. Machapisho haya yanapaswa yapatikane katika mazingira ili kum saidia mwalimu asitumie muda au gharama nyingi ku yatafuta pale atakapokuwa ~~na~~ anayahitaji. Sifa kubwa ya machapisho haya ni kupatikana katika mazingira lengo ni kumwezesha mtu yeyote anayetaka kuyatu mia ayapate kwa urahisi.

Yazingatie Lugha fasaha. Pia Mwalimu anapochagua Machapisho haya anachoangalia zaidi ni lugha inayoeleweka, Machapisho yanapaswa yatumie Lugha inayoeleweka, isiwe lugha ngumu ambayo itamfanya msomaji asielewe, Kila mtu anapotaka kuyatumia inamfanya kuhamasika kuendelea kuya tumia. Hivyo basi, lugha ndiyo nyenzo kuu ya mawasiliano

Yaendane na Umahiri husika. Pia mwalimu anapaswa kuchagua machapisho yanayoendana na umahiri mfano Mada za Somo la Uraia ziendane na machapisho ya Uraia kadhalika ~~kw~~ vivyo hivyo na masomo mengine yapasa yazingatie machapisho yake. Machapisho yasipo endana na Umahiri husika inakuwa vigumu kuya tumia kwani yatakuwa hayana kidhi kiwango na shughuli inayopaswa kutendeka au kufanywa.

11 Cont.

Yawe na Uhalisia: Mwalimu anapokuwa anachagua machapisho haya yanapaswa yazingatie uhalisia yasiwe ya kubuni. Hapa Mwalimu azingatie Viwango vi-na Vigezo Vya Uchaguzi wa Machapisho, Kwani asipokuwa makini anaweza akapata machapisho ya kubuni, Machapisho ambayo si halisi huwa na lugha tofauti na Machapisho halisi pia yanachakaa mapema. Hivyo basi uhalisia unaweza kuonekana pale ambapo Umakini wakati wa Uchaguzi utawekwa.

Yasitumie lugha ya Upendeleo na Yaendane na mahitaji ya walengwa. Mfano wa lugha ya upendeleo ni kama vile matusi: Uchaguzi wa Machapisho haya unazingatia mno lugha. Ili chapisho lolote lionekane na Viwango lazima lizingatie lugha ambapo basi lugha ndiyo nyenzo kuu ya mawasiliano, Lugha ikiwa fasaha ingejenga mawasiliano mema, Ufasaha wa kitu hubebwa na Lugha. Machapisho yakiwa na lugha ya matusi au ya Upendeleo Inakuwa Vigumu kutumika hasa wakati wa ufundishaji na Ujifunzaji

Kwahiyo; Kuna Hm Siyo sifa tu za machapisho ya Somo la Uraia bali kuna Umuhimu wa kutumia Machapisho haya mfano. Humpatia mtoto maarifa mapya, Humpatia mtoto Uwezo wa Kutunza kumbukumbu, Uwezo wa kufikiri, Ni njia mojawapo ya kufahamu mambo mapya na kupata ujuzi

**Kielelezo Na. 11.1:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 11.

Aidha, watahiniwa 1,645 (28.2%) waliopata alama 6 hadi 10 katika swali hili walikuwa na maarifa ya wastani katika dhana ya sifa za machapisho bora zitakazomwezesha mwalimu kuchagua machapisho bora katika muktadha wa somo la Uraia. Baadhi yao, walitoa hoja pungufu ya tano zisizokuwa na mtiririko mzuri. Aidha, wengine hawakuwa na utangulizi wala hitimisho na walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja, mbali na kutoa hoja sahihi, alitoa pia hoja zisizo sahihi ambazo ni *machapisho bora lazima yawe na fremu* na

*machapisho yanatakiwa yawe na maneno mafupi au yasiwe na maneno.* Majibu hayo yanaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu sifa za machapisho zitakazomwezesha mwalimu kuchagua machapisho bora katika muktadha wa somo la Uraia.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 395 (6.8%) waliopata alama 0 hadi 5.5 walikuwa na maarifa hafifu juu ya sifa za machapisho yanayotumika katika ufundishaji na ujifunzaji. Baadhi yao, walitoa hoja zenye maelezo dhaifu na wengine walitaja hoja bila utangulizi, ufafanuzi wala hitimisho. Watahiniwa waliopata alama 0 walikosa maarifa juu ya sifa zinazomwezesha mwalimu kuzingatia wakati wa kuchagua machapisho bora. Wengi wao hawakuandika majibu na baadhi yao walitoa hoja zisizo sahihi kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika hoja kama vile *machapisho bora lazima yawe na maswali, machapisho bora lazima yawe na kichwa cha mada,* na *machapisho bora lazima yawe na mwaka wa kuandikwa kwa machapisho hayo, mfano 1982.* Mtahiniwa mwingine aliandika hoja kama vile *machapisho lazima yaendane na mila na desturi za mahali au eneo husika, machapisho yanahitajika ili wanafunzi waweze kusoma matini,* na *machapisho huchochea ari kujifunza kwa mwanafunzi.* Kielelezo Na. 11.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.


11 Machapisho bora ;ni hali ya kutenda jambo au mambo ya mandiko tofautitofauti kama vile majarida, makala, na magazeti. Zifuatazo ni hoja tano za sifa zinazochanga zikazo mesha mwalimu kuchangua machapisho bora katika muktadha wa somo la Uraia.

Kuwepo na semina mbalimba linalohusiana na machapisho bora ;ni muhimu kwani mwalimu hufanya tathmini ya kutambua vigezo na viwango vya machapisho bora yatayotumika katika somo la uraia.

Kupitia elimu ya masafa yaani mitandaoni ;mwalimu kuwa mbunifu kulingana ukuwaji wa sayansi na teknolojia. hivyo mwalimu hana budi kutochagua machapisho bora ya ufundishaji katika somo la Uraia.

Kupitia maudhurio ya maktaba ;husaidia kupata machapisho bora kwa utapata maarifa, ujuzi na stadi kwenye suala la elimu. kuweza kuwepo na rejea nyingi za kufundishia somo la uraia.

Kupitia makongamano ya taaluma ya elimu ;mwalimu itamuwezesha kujikita na maendeleo ya kuleta maendeleo ya aina tofautitofauti. mwalimu ataweza kujipatia machapisho bora ya kufundishia somo la uraia.

Kupitia udumaji wa majarida na makala mbalimbali za machapisho ; Mwalimu ataweza kuchambua maudhui mapya na mazuri yatayo muwezesha kupata machapisho bora.

Hitimisho ; Ni muhimu mwalimu kufanya tathmini kwa kile atakacho fanyia utafiti kama kina weza kufanya vizuri kuchangua machapisho bora kwa kufuata vigezo vyote vya kupata machapisho bora ya kusoma na kundishia somo la uraia.

**Kielelezo Na. 11.2:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 11.

Katika Kielelezo Na. 11.2, mtahiniwa alieleza mahali au namna ambavyo machapisho yanaweza kupatikana badala ya kueleza sifa zitakazomwezesha mwalimu kuchagua machapisho bora katika muktadha wa somo la Uraia. Aidha, mtahiniwa aliandika utangulizi na hitimisho lisilo sahihi.

### 2.2.2 Swali la 12: Upimaji na Tathmini

Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza faida tano za matokeo ya upimaji kwa mwalimu. Kati ya watahiniwa 5,822 (100%) waliofanya swali hili, watahiniwa 32 (0.5%) walipata alama 0 hadi 5.5, watahiniwa 449 (7.8%) walipata alama 6 hadi 10, na watahiniwa 5,341 (91.7%) walipata alama 10.5 hadi 15. Kwa ujumla swali

hili lilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kuwa watahiniwa 5,790 (99.5%) walipata alama 6 hadi 15. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 12.




**Chati Na. 12:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 12*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 5,341 (91.7%) waliopata alama 10.5 hadi 15 walikuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana ya upimaji hasa katika kipengele cha matokeo ya upimaj wa kielimu. Aidha, walielewa matakwa ya swali hivyo, walitoa hoja sahihi na zenye mantiki. Baadhi ya majibu sahihi yaliyotolewa katika swali hili ni *humsaidia mwalimu kujua changamoto za ufundishaji na ujifunzaji, humsaidia mwalimu kujua maendeleo ya wanafunzi wake katika tendo zima la ufundishaji na ujifunzaji, humsaidia mwalimu kuboresha ufundishaji wake,* na *humsaidia mwalimu kuamua zana/vifaa gani vya kufundishia na kujifunzia vitumike*. Kielelezo Na. 12.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

**12**

Upimaji ni mchakato wa kukusanya, kuchambua na kutafsiri matokeo au taarifa kwa ajili ya kutoa maamuzi sahihi. Zifuatazo ni faida za matokeo ya upimaji kwa mwalimu kama ifuatavyo:-

Humsaidia mwalimu kujua uelewa wa mwanafunzi; Mwalimu anapotunza matokeo ya upimaji wa elimu unamsaidia mwalimu kujua uelewa alionao mwanafunzi ili kupima katika ujifunzaji wake.

Pia humsaidia mwalimu kuchagua mbinu sahihi; Mwalimu upimaji anaweza kuchagua mbinu ambayo mwanafunzi aweze kuelewa zaidi kupitia matokeo ambayo anayafanya katika ufundishaji wake.

Humsaidia mwalimu kutatua changamoto anazokutana nazo Mwanafunzi; Mwalimu anaweza kutatua changamoto za mwanafunzi kupitia matokeo ya upimaji wa elimu.

Inamrahisishia mwalimu kujua wanafunzi wanaoendelea; Matokeo ya upimaji katika Elimu yanamsaidia mwalimu kujua wanafunzi ambaye ataendeleo na masomo wakati wa kufanya maamuzi sahihi.

Humsaidia mwalimu kutoa taarifa za maendeleo ya elimu kitaifa; Mwalimu anaweza kufanya tathimini ili aweze kutoa taarifa za maendeleo ya mwanafunzi za elimu kitaifa ili aweze kufanikisha madhumuni yake ya matokeo ya upimaji kwa mwalimu

**12 Cont.**

Hivyo basi katika faida za matokeo ya upimaji ni lazima changamoto zijitikeze katika matokeo ya upimaji kama kushindwa kufanya tathmini pia matokeo kutokuwa sahihi

**Kielelezo Na. 12.1:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 12.

Aidha, baadhi ya watahiniwa 449 (7.8%) waliopata alama 6 hadi 10 katika swali hili, walishindwa kutoa maelezo sahihi katika kutetea baadhi ya hoja zao na wengine walishindwa kutoa utangulizi na hitimisho lenye kujitosheleza. Miongoni

mwao, wapo walioandika hoja pungufu na wengine walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika hoja kama vile: *matokeo ya upimaji husaidia kutambua changamoto za ujifunzaji* na *kufanya tathmini ya ufundishaji na ujifunzaji* bila maelezo ya kina kutetea hoja hizo. Majibu hayo yanaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu faida za matokeo ya upimaji kwa mwalimu.

Kwa upande mwingine, kati ya watahiniwa 32 (0.5%) waliokuwa na ufaulu hafifu, hakuna mtahiniwa aliyepata alama 0. Watahiniwa katika kundi hili walipata alama kuanzia 1 hadi 5.5 kwa kuwa walikuwa na maarifa hafifu kuhusu faida za matokeo ya upimaji kwa mwalimu. Wengi wao walitoa hoja zisizo sahihi kinyume na matakwa ya swali. Baadhi yao walijibu swali bila kuanza na utangulizi, ufafanuzi wa kina wa hoja wala hitimisho lenye kuakisi hoja zilizotolewa. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika: *matokeo ya upimaji wa kielimu unamsaidia mwanafunzi kupata vyeti, upimaji unampa mwanafunzi ari ya kujifunza,* na *husaidia mwanafunzi kuhama darasa na kwenda ngazi ya juu ya elimu.* Mtahiniwa mwingine aliandika: *matokeo ya upimaji humjengea mwanafunzi kumbukumbu ya kudumu, humfanya alipende somo pamoja na mwaalimu wake wa somo,* na *huongeza ushirikiano darasani katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji*. Kielelezo Na.12.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.



12 Upimaji, ni mchakato au kitendo cha kuangalia ni kwa namna gani mwanafunzi amekuwa kupata maarifa na ujuzi alio fundishwa kuna aina nyingi za upimaji ambazo ni upimaji awali, endelevu, tahizi na tamati. Zifuatazo ni faida za matokeo ya upimaji wa kielimu.

Humsaidia mwalimu kuboresha mbinu za kufundishia na kujifunzia, hii ndo faida ya kwanza ya matokeo ya upimaji" kwani humsaidia mwalimu kuboresha mbinu za kufundishia na kujifunzia.

Husaidia wahitimu kupata ajira, pia na hii ni mojawapo ya faida za matokeo ya upimaji wa elimu kwani huweza kusaidia wahitimu kujiunga na ajira.

Husaidia kuamsha hari ya kujifunza kwa wanafunzi, pia na hii ni faida nyingine ya matokeo ya ya upimaji kwani huweza kuamsha hari ya kujifunza kwa wanafunzi" waliofanya vizuri na ambao hawajafanya vizuri.

Huweza kupelekwa darasani na kujadiliwa pia na hii ni faida nyingine ya matokeo ya upimaji kwani huweza kupelekwa darasani na yakajadiliwa ili kubaini dosari zilizojitokeza na jinsi ya kuzifuta dosari hizo.

Husaidia mwanafunzi kuhama ngazi moja ya elimu kwenda ngazi nyingine, pia na hii ni umuhimu mwingine wa matokeo ya upimaji kwani huweza kumfanya kuhama kutoka ngazi moja ya elimu kwenda ngazi nyingine.

Hitimisho, matokeo ya upimaji wa kielimu

12 Cont. yana faida nyingi sana mbali na nilizozitaja hapo juu mfano kujua nafasi ya shule kitaaluma.

**Kielelezo Na. 12.2:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 12.

Katika Kielelezo Na. 12.2, mtahiniwa alitoa hoja tano za matokeo ya upimaji. Hoja ya kwanza ilikuwa sahihi na hoja zingine nne zilihusu faida za matokeo ya upimaji kwa mwanafunzi badala ya kueleza faida za matokeo ya upimaji kwa mwalimu, hivyo alipata ufaulu hafifu.

### 2.2.3 Swali la 13: Maandalizi ya Kufundisha Somo la Uraia

Swali lilimtaka mtahiniwa kueleza manufaa matano ya kutumia mbinu shirikishi ya maswali na majibu katika ufundishaji na ujifunzaji. Watahiniwa 5,822 (100%) walijibu swali hili ambapo watahiniwa 124 (2.1%) walipata alama 0 hadi 5.5, watahiniwa 2,519 (43.3%) walipata alama 6 hadi 10, na watahiniwa 3,179 (54.6%) walipata alama 10.5 hadi 15. Kwa ujumla, swali hili lilikuwa na ufaulu mzuri kwa kuwa watahiniwa 5,698 (97.9%) walipata alama 6 hadi 15. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 13.




**Chati Na. 13:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 13*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa katika swali hili unaonesha kuwa watahiniwa 3,179 (54.6%) waliopata alama 10.5 hadi 15 walieleza kwa usahihi manufaa matano ya mbinu shirikishi ya maswali na majibu katika ufundishaji na ujifunzaji. Watahiniwa hao walidhihirisha kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada ya maandalizi ya kufundisha somo la Uraia na walielewa vema matakwa ya swali kwa kuwa walitoa hoja na ufafanuzi wenye mtiririko mzuri. Majibu sahihi yaliyotolewa ni *husaidia kujenga kumbukumbu ya kudumu au muda mrefu kutokana na ushiriki wa mwanafunzi katika somo, husaidia wanafunzi kufikiri kwa kina kwani mwanafunzi anapododosa huibua fikra tunduizi kwao, mwalimu anapouliza maswali inamsaidia kuwafahamu wanafunzi wake na wanafunzi kujisika vizuri na hujisikia kupendwa na mwalimu pale wanapojibu/kuuliza swali, mbinu hii ya maswali na majibu humsaidia mwanafunzi kujifanyia tathmini yeye mwenyewe katika mchakato mzima wa ujifunzaji wake hasa wakati anapouliza na kujibu swali,* na *huamsha ari ya kujifunza na huongeza utulivu darasani*. Majibu

mengine sahihi yaliyotolewa yalikuwa ni *mbinu hii ya maswali na majibu huchochea udadisi kwa mwanafunzi katika mchakato mzima wa ufundishaji na ujifunzaji, husaidia wanafunzi kujenga stadi ya kujiamini anapoweza kujibu au kuuliza swali darasani, huweza kumrahisishia mwalimu kazi ya ufundishaji,* na *mwalimu atakuwa na maneno machache ya kuzungumza darasani ambapo sehemu kubwa ya mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji itafanywa na wanafunzi wenyewe.* Kielelezo Na. 13.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

13

Maswali na majibu ni mbinu shirikishi ambayo humshirikisha mwanafunzi katika kujifunza, kwasababu katika mbinu hii mwalimu anauliza maswali na kuwataka wanafunzi kujibu kitu alichowauliza. Ni kweli kwamba dhana ya hapi na majibu imefundishwa na kueleweka kwa kutumia mbinu shirikishi ya maswali na majibu. Yafuatayo ni manufaa ya kutumia mbinu ya maswali na majibu.

Kuwajengea wanafunzi kumbukumbu ya kudumu; mbinu ya maswali na majibu huwajengea wanafunzi kumbukumbu ya kudumu kwasababu mwanafunzi anapojaribu kujibu swali itamsaidia kujua makosa yake na mwalimu atakapomrekebisha itakuwa ni vigumu kwa mwanafunzi huyo kusahau au kurudia makosa, kwahiyo mwanafunzi anapojaribu humpelekea kukumbuka kitu alichojifunza.

Husaidia kuchochea udadisi kwa wanafunzi; pia mwalimu anapotumia mbinu ya maswali na majibu husaidia kuchochea udadisi kwa wanafunzi kwasababu mwalimu anapouliza swali anatarajia kupata jibu kutoka kwa wanafunzi hivyo wanafunzi hawana budi kufikiria kitu kwa undani ili waweze kupata jibu, hivyo mbinu hii huwafanya wanafunzi kuwa wadadisi wa mambo mbalimbali na inawajengea wanafunzi uwezo wa kufikiri zaidi

Husaidia kuvuta usikivu kwa wanafunzi; mbinu ya maswali na majibu husaidia kuvuta usikivu wa wanafunzi wanafunzi wanatakiwa kuwa makini katika kusikiliza kitu kinachoulizwa ili aweze kuelewa kitu hicho lakini kama mwanafunzi hatakuwa makini katika kusikiliza hataweza kuelewa kitu kinachoulizwa. Kwahiyo mbinu ya maswali na majibu humjengea mwanafunzi au humsaidia mwanafunzi

| 13 Cont. | Kuvuta usikivu au kuwa makini ili aweze kusikia na swali yanayoulizwa kwa makini zaidi |
|---|---|
| | Husaidia kurahisisha ufundishaji na ujifunzaji. - Mbinu ya maswali na majibu humpunguzia mwalimu kutumia nguvu nyingi katika kufundisha kwasababu mbinu hii humshirikisha mwanafunzi pia hivyo mwalimu anapopata majibu ya maswali aliyowauliza wanafunzi hatatumia ~~mbinu~~ nguvu nyingi sana katika kueleza au kufundisha kwasababu hupata maarifa kutoka kwa wanafunzi wenyewe. |
| | Huamsha ari ya mwanafunzi kujifunza na kulipenda somo; kwasababu mwanafunzi anapokuwa mtendaji katika kujifunza anakuwa hachoki haraka katika ujifunzaji wake, kuliko akiwa ni msikilizaji tu. Hivyo kwasababu mbinu hii humshirikisha mwanafunzi kujifunza hivyo kumfanya mwanafunzi kuwa na ari ya kujifunza na hata ~~ata~~ kuwa analipenda somo. |
| | Kwahiyo mbinu ya maswali na majibu ni muhimu kabisa katika ufundishaji lakini isipotumika vizuri inaweza ikapelekea mwalimu kushindwa kufikia malengo yake, pia inaweza kusababisha kelele darasani. |

**Kielelezo Na. 13.1:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 13.

Aidha, watahiniwa 2,519 (43.3%) waliopata alama 6 hadi 10 katika swali hili, majibu yao yalikuwa na mapungufu mbalimbali kama vile kuchanganya maelezo sahihi na yasiyo sahihi, kutoa hoja zisizokuwa na ufafanuzi wa kina, na utangulizi au hitimisho lisilojitosheleza. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa majibu kama ifuatavyo: utangulizi- *mbinu ni jumla ya shughuli au njia zote anazotumia mwalimu ili kuweza kufundishia darasani.* Manufaa ya mbinu ya maswali na majibu ni *kukuza uwezo wa kufikiri kwa mwanafunzi, humsaidia mtoto kuweza kujifunza misamiati,* na *humsaidia mwalimu kufundisha kwa urahisi na haraka*. Majibu hayo yanaonesha kuwa watahiniwa hao hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu manufaa ya mbinu shirikishi ya maswali na majibu katika ufundishaji na ujifunzaji.

Hata hivyo, baadhi ya watahiniwa 124 (2.1%) waliopata alama 0 hadi 5.5 katika swali hili, hawakuwa na maarifa ya kina kuhusu dhana iliyoulizwa na hivyo walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi. Watahiniwa waliopata alama 0, baadhi yao hawakuandika majibu. Hii inaonesha kuwa hawakuwa na maarifa kabisa ya dhana iliyoulizwa. Wengine hawakuelewa matakwa ya swali hivyo kuandika majibu yasiyohusiana na swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja aliandika mambo

ambayo yanaweza kujitokeza endapo haki na wajibu vitafuatwa na kuzingatiwa kama ifuatavyo: *inaweza kuondoa matabaka miongoni mwao, inaondoa upendeleo, husababisha uwepo wa utawala bora, upatikanaji wa huduma bora za jamii,* na *kuondoa unyanyasaji*. Pia, baadhi ya watahiniwa walishindwa kutoa utangulizi na hitimisho linaloendana na matakwa ya swali, hivyo walipata alama hafifu. Kielelezo Na. 13.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.

**13** Haki; ni mambo yote stahiki anayotakiwa kufanyiwa raia kwa mujibu wa Sheria. Wajibu ni mambo yote anayotakiwa kuyafanya mtu bila kuvunja Sheria. Kilo kana kwa dhana ya haki na wajibu imefundishwa na kueleweka kwa kutumia mbinu Shirikishi ya maswali na majibu kuna manufaa yaliyopatikana katika kutumia mbinu hiyo. Ufuatao ni manufaa ya kutumia mbinu hiyo.

Humwezesha kila raia kushiriki kikamilifu mbinu hii mamsaidia ata raia wa hali chini kushiriki kikamilifu katika kujua haki na wajibu wake.

Husaidia kuondoa unyanyasaji; Kupitia mbinu hii katika kuelekeza na kufundisha dhana ya haki na wajibu imesaidia sana kuondoa unyanyasaji wa watu wa hali za chini sana.

Husaidia kuondoa Upendeleo, Mbinu hii imeweza kuondoa kabisa hali ya Upendeleo kwa kila raia katika kushiriki vyema kuchangia kuusu dhana ya haki na wajibu wake.

Husaidia kuondoa matabaka; Katika kufundisha na kuelekeza dhana hii ya haki na wajibu kwa kutumia hiyo mbinu ya Shirikishi ya maswali na majibu kumesaidia sana kuondoa matabaka mbayo yangeweza kuwepo kwa watu na Serikali.

Husaidia kupunguza malalamiko; Kupitia mbinu hii ya kushiriki ya maswali na majibu Mbinu hii imeweza kuondoa malawamo ambayo yangeweza kujitokeza kwa Serikali.

Hivyo basi; Kila raia wa Tanzania lazima apewe haki zake zote anazostahili na yeye kutimiza na kufanya mambo yake bila kwenda kinyume na Sheria za nchi ya Tanzania.

**Kielelezo Na. 13.2:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 13.

Katika Kielelezo Na. 13.2, mtahiniwa alieleza manufaa ya utekelezaji wa haki na wajibu badala ya kueleza manufaa ya kutumia mbinu shirikishi ya maswali na majibu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

### 2.2.4 Swali la 14: Uchambuzi wa Maandiko/Machapisho Muhimu ya Kufundishia/Kujifunzia Somo la Uraia

Swali lilimtaka mtahiniwa kuthibitisha kwa hoja tano umuhimu wa kiongozi cha Mwalimu kama mwongozo unaomwezesha mwalimu kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Watahiniwa 5,822 (100%) walijibu swali hili, ambapo watahiniwa 13 (0.2%) walipata alama 0 hadi 5.5, watahiniwa 1,140 (19.6%) walipata alama 6 hadi 10, na watahiniwa 4,669 (80.2%) walipata alama 10.5 hadi 15. Kwa ujumla swali hili lilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu kwa kuwa watahiniwa 5,809 (99.8%) walipata alama 6 hadi 15. Muhtasari wa kiwango cha ufaulu katika swali hili umeoneshwa katika Chati Na. 14.




**Chati Na. 14:** *Ufaulu wa Watahiniwa katika Swali la 14*

Uchambuzi wa majibu ya watahiniwa unaonesha kuwa watahiniwa 4,669 (80.2%) waliopata alama 10.5 hadi 15 walithibitisha kwa usahihi kuwa kiongozi cha mwalimu ni mwongozo muhimu unaomwezesha mwalimu kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Watahiniwa hao walikuwa na uelewa wa kutosha katika mada ndogo ya uchambuzi wa kiongozi cha mwalimu kwa kueleza kwa usahihi umuhimu wa kiongozi cha mwalimu kama vile *humsaidia mwalimu kufundisha na kufanya upimaji, humwelekeza mwalimu namna ya kutumia kitabu cha kiada, humsaidia mwalimu kufundisha mada husika na ujuzi unaotakiwa kujengwa,*

*humsaidia kujua muda unaotakiwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa mada husika,* na *humsaidia kuchagua mbinu na njia stahiki za ufundishaji wa mada husika*. Kielelezo Na. 14.1 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyejibu swali hili kwa usahihi.

14 KIONGOZI CHA MWALIMU; Ni kitabu ambacho
cho anakitumia mwalimu katika tendo zima la
ufundishaji na humpa mwongozo juu ya nini ha
kifundishe kwa muda maalumu darasa maalumu
na mada maalumu walengwa maalumu.
Nathibitisha kauli ya kwamba kiongozi
cha mwalimu ni mwongozo muhimu ambao
unamuwezesha mwalimu kutekeleza majukumu
yake kama ifuatavyo (Nakubali);
Kiongozi cha mwalimu humsaidia m
walimu kutambua zana za ufundishaji; Tunap
ozungumzia zana hii ina maana ya vifaa jumla
ya vifaa vyote ambavyo mwalimu anavitumia
katika tendo zima la ufundishaji darasani
ndo zana hivyo kiongozi kina mwongozo pale
kwamba mada fulani mwalimu unapaswa ut
umie zana hizi hapa Mfano Utamaduni kitemu
elekeza atumie vitu halisi / Michoro / picha au
vifani vya mavazi ya kiutamaduni humsaidia ku
tambua zana za ufundishaji.
Kiongozi cha mwalimu humsaidia
mwalimu kufundisha kwa kufuata hatua za
somo; Hapa ina maana katika kiongozi kuna seh
emu ya hatua za somo hapo ataanza kumueleze
a mwalimu afuate hatua zipi Mfano Mada ya
Mawasiliano hatua 01/ kumuongoza mwalimu kuwa
za maana ya mawasiliano 02/ kuwaongoza wanafunzi
kutaja vifaa vya mawasiliano 03/ kuwaongoza wanaf
unzi kutaja / kuorodhesha Matumizi vifaa hivyo
hivyo ndivyo kinavyomsaidia mwalimu kufun
disha kwa kufuata hatua za somo husika.

14 Cont.

Kiongozi cha mwalimu humsaidia Mwalim
u Kujua njia / mbinu atakayotumia Kufundishia som
o lake ; Katika kitabu cha Kiongozi cha mwali
mu Kinakupa mwongozo Kwamba utumie mbinu
au njia ya majadiliano (Vikundi Vidogovidogo) au
mbinu ya changanyaketo ili uweze Kufundisha
somo lako vizuri na wanafunzi waweze kukuelewa
nini unachokifundisha Kulingana na Mada yako.

Kiongozi cha Mwalimu humsaidia mwali
mu Kupata mazoezi ya kutoa ~~wakati~~ baada kufundisha
na atakapomaliza Kufundisha na Majibu yake ; kit
abu hiki kina maswali yanayompima mwanafunzi
juu ya kile alichofundishwa amekielewa na maswa
li hayo yapo na majibu yake mwishoni hapohapo
hivyo mwalimu hana kazi ya kutafuta majibu k
wani majibu hayo kashayapata yapo katika kitabu

Kiongozi cha Mwalimu humsaidia mwa
limu katika usahihishaji wa mazoezi aliyotoa kuto
kana majibu yake yapo palo chini ya maswali ; pale
mwalimu anapotaka kusahihisha zoezi alilotoa
majibu yatakuwa yapo chini ya zoezi lile hivyo
yeye hana kazi ya kutafuta majibu ya maswali
yale zaidi ya kufundisha kusahihisha kazi aliyo
wapa wanafunzi wake darasani.

Kiongozi cha Mwalimu humsaidia mwa
limu Kuandaa Andalio la somo ; sababu kupitia
kiongozi kuna hatua za ufundishaji kuna zana za
ufundishaji kuna mbinu kuna mada na Andalio la
somo kuna shughuli kuu (Mada kuu) na shughuli mahu
susi < Mada ndogo) zana (kuimarisha umahiri) kuna
Tathmini (mbinu ulizotumia katika ufundishaji pia hun
eza kuandaa kupitia kiongozi cha Mwalimu inawezekana.



14 Cont. Hivyobasi; Huo ndio umuhimu wa kiongozi cha mwalimu kuthibitisha uongozi wake licha ya kuwa kiongozi lakini pia kiongozi cha mwalimu kina mapungufu yake ikiwemo hakina picha michoro au kielelezo cha aina yoyote ile ambacho kitatumika katika tendo zima la ufundishaji na la ujifunzaji, kiongozi ni kitabu ambacho hutumiwa na mwalimu tu hivyo kina ubaguzi mwanafunzi haruhusiwi kutumia pia kiongozi hakina mpangilio mzuri wa mada kwa mtiririko mada zake zime changanywa hazijapangiliwa na kiongozi hakimu hitaji [illegible] mwanafunzi akitumie ni mwalimu tu.

**Kielelezo Na. 14.1:** Sampuli ya jibu sahihi katika swali la 14.

Aidha, watahiniwa 1.140 (19.6%) waliopata alama 6 hadi 10 katika swali hili, baadhi yao walianza na utangulizi sahihi na kutoa hitimisho kama inavyopaswa lakini walieleza hoja dhaifu au pungufu kulingana na matakwa ya swali. Wengine walichanganya hoja sahihi na zisizo sahihi na pia hawakuweza kufafanua hoja katika mtiririko wenye mantiki. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja tatu ambazo ni *hupendekeza mbinu ya ufundishaji, hutoa majibu ya mazoezi yaliyo katika kitabu cha kiada,* na *huonyesha mpangilio na mtiririko wa ufundishaji.* Mtahiniwa mwingine alitoa hoja mbili ambazo ni *husaidia mwalimu kupata maarifa mapya* na *husaidia mwalimu kujiamini wakati wa kufundisha*. Aidha, alitoa hitimisho ambalo ni *kutokana na hayo mwalimu anapaswa kutumia kiongozi cha mwalimu kwa sababu huonesha zana na maswali yote yaliyopo kwenye kitabu cha kiada wakati wa kusahihisha maswali hayo*. Majibu hayo yanaonesha kuwa watahiniwa katika kundi hili hawakuwa na maarifa ya kutosha kuhusu umuhimu wa kiongozi cha mwalimu kama mwongozo unaomwezesha mwalimu kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Kwa upande mwingine, watahiniwa 13 (0.2%) waliopata alama 0 hadi 5.5 walikuwa na maarifa hafifu kuhusu dhana ya umuhimu wa kiongozi cha Mwalimu. Baadhi yao waliandika utangulizi au hitimisho lenye mapungufu, walichanganya majibu sahihi na yasiyo sahihi na maelezo hayakuwa na mtiriko mzuri. Watahiniwa waliopata alama 0 hawakuwa na maarifa kabisa kuhusiana na dhana iliyoulizwa hivyo kuandika majibu yasiyo sahihi. Hivyo, hawakuelewa matakwa ya swali. Kwa mfano, mtahiniwa mmoja alitoa hoja zisizo sahihi kama vile *muhtasari, kitabu cha kiada,* na *kiongozi cha mwalimu kama mwongozo wa ufundishaji*. Pia, mtahiniwa mwingine alitoa hoja zisizo sahihi ambazo ni

*mazingira ya kujifunzia watoto wanapokuwa shuleni, kuandaa hadithi za watoto, mbinu mbalimbali, mwalimu kutatua changamoto zote na kujua majukumu yake,* na *kusahihisha kazi anazowapatia watoto*. Kielelezo Na. 14.2 ni sampuli ya jibu la mtahiniwa aliyeshindwa kujibu swali hili kwa usahihi.

**14 Cont.**

Kiongozi: Ni Mtu anaye husika katika kusimamia na kuendeleza Sheria za nchi fulani katika Muongozo wa Mwalimu Unaonyesha kiongozi cha Mwalimu katika Utekelezaji wa Majukumu ya Mwalimu katika ~~Na~~ Uendeshaji kazi wake katika kufundisho somo la uraia.

Kuandaa Mazingira ya kujifunzia watoto Wanapokua Shuleni kwenye somo la uraia, katika Mazingira yanayo Mzunguko Mtoto Mwalimu huma kuwa na Majukumu ya kuandaa mazingira ya kujifunzia darasani

Kuandaa hadithi za watoto; Mwalimu katika kutekeleza majukumu yake lazima aandae hadithi ambazo zitawafanya watoto waweze kujifunza ipasavyo na kuongozwa na kiongozi cha mwalimu ambacho humuelekeza mwalimu kuwa kufundisha somo lake.

Kuandaa Mbinu Mbalimbali za kufundisha na kujifunzia somo la uraia: Mwalimu ni muhimu kufahamu Majukumu yake ipasavyo katika uandaaji wa zana ambazo zitamsaidia mwalimu katika Shughuli za ufundishaji

~~Husaidia kumwongoza mwalimu maarifa~~

Kusajili watoto Shuleni. Mwalimu husaidiwa na kiongozi ~~cha~~ ambacho huweza kumsaidia mwalimu kutatua changamoto zote na kuweza kujua majukumu yake ya Shuleni anapokuwa Shuleni katika kutekeleza mambo mbalimbali yanayoikabili Shule.

Kufanya kazi anazopewa na mwalimu Mkuu; Mwalimu huweza kuzingatia baadhi


14 Cont.
ya mambo ambayo huweza kumsaidia mtoto kushi-
riki kufanya shughuli mbalimbali ambazo zina
husiana na shule na kukabiliana nazo
Kusahihisha kazi zao au wapatia wadau; Mwali-
mu kutima atatambua majukumu yake katika
kiongozi wake hii huweza kumsaidia mwalimu
kutimiza wajibu wake wa kusahihisha kazi zao
wapatia wadau darasani
Hivyo Kiongozi cha mwalimu ni mwongozo
muhimu unaomwezesha mwalimu kutekeleza majukumu
yake ipasavyo yakiwatayo ni majukumu ya mwali-
mu katika kutekeleza majukumu wa majukumu yake
anapokua shuleni humsaidia kuweza kufanya baadh-
ya vitu mbalimbali anapokua shuleni.

**Kielelezo Na. 14.2:** Sampuli ya jibu lisilo sahihi katika swali la 14.

Katika Kielelezo Na. 14.2, mtahiniwa alieleza dhana mbalimbali zinazotumiwa na mwalimu katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji badala ya kueleza umuhimu wa Kiongozi cha mwalimu kama mwongozo unaomwezesha mwalimu kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

## 3.0 UCHAMBUZI WA UFAULU WA WATAHINIWA KWA KILA MADA

Mtihani wa somo la Uraia ulitahini mada nane (08). Uchambuzi wa takwimu za matokeo umeonesha kuwa mada saba (7) kati ya nane (08) zilikuwa na kiwango kizuri cha ufaulu. Mada hizo ni: *Upimaji na Tathmini (99.5%), Utamaduni wetu (97.4%), Uchambuzi wa Maandiko/Machapisho muhimu ya kufundishia somo la Uraia (96.5%), Maandilizi ya kufundisha somo la Uraia (96.3%), Uchumi wetu (91.3%), Misingi ya ufundishaji wa somo la Uraia (87.1%)* na *Dola (78.1%)*. Ufaulu huu umesababishwa na watahiniwa wengi kuwa na maarifa ya kutosha kuhusu mada zilizoulizwa na uwezo wa kutafsiri kwa usahihi matakwa ya swali. Hata hivyo, mada ya *Zana za Kufundishia na Kujifunzia* ilikuwa na kiwango cha wastani cha ufaulu wa asilimia 66.1. Ufaulu huo umetokana na watahiniwa wengi kutokuwa na maarifa ya kutosha na umahiri wa kuandika hoja zenye mtiririko mzuri kimantiki katika mada hiyo hususani mada ndogo ya *Aina ya zana*. Muhtasari wa ufaulu wa mada umeoneshwa katika Kiambatisho A.

Uchambuzi zaidi ulifanyika kwa kuangalia ulinganifu wa kiwango cha ufaulu wa mada kati ya mwaka 2022 na 2023. Ilibainika kuwa kiwango cha ufaulu katika mada za *Upimaji na Tathmini, Utamaduni Wetu, Uchambuzi wa Maandiko/Machapisho muhimu ya kufundishia somo la Uraia, na Maandilizi ya kufundisha somo la Uraia* kiliongezeka kwa asilimia 23.8, 22.14, 18.9 na 9.24 mtawalia. Aidha, uchambuzi wa kiwango cha ufaulu cha mada za *Uchumi Wetu*, *Dola* na *Zana za Kufundishia na Kujifunzia* umeonesha kushuka kwa asilimia 8.1, 18.8 na 3.0 mtawalia. Ulinganifu wa ufaulu wa mada kati ya mwaka 2022 na 2023 umeoneshwa katika Kiambatisho B.

## 4.0 HITIMISHO

Ufaulu wa watahiniwa katika Mtihani wa Uraia mwaka 2023 ni mzuri kwa kuwa watahiniwa 5,753 (99.97%) walipata ufaulu mzuri. Ufaulu huu mzuri umetokana na watahiniwa kuwa na maarifa ya kutosha kwenye vipengele vingi vya mada zilizotahiniwa. Walio wengi walielewa vema matakwa ya swali na kutoa hoja sahihi zenye ufafanuzi wenye mtiririko mzuri. Aidha, ufaulu wa mwaka 2023 umeongezeka kwa asilimia 0.16 ukilinganisha na ufaulu wa mwaka 2022 ambapo watahiniwa 4,635 (99.81%) walifaulu vizuri.

## 5.0 MAPENDEKEZO

Ili kuongeza kiwango cha kufaulu katika mada yenye ufaulu wa wastani hususani mada ndogo ya *Aina ya Zana,* yafuatayo yamependekezwa:

(a) Wakufunzi watumie zana kuona (picha na michoro), kusikia (redio) pamoja na zana za kuona na kusikia (televisheni) wakati wa mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji ili kuwajengea umahiri wa *Aina ya Zana*.

(b) Ufundishaji na ujifunzaji wa mada ndogo ya *Aina ya Zana* utumie mbinu shirikishi kama vile majadiliano katika vikundi, mdahalo, kisa mafunzo, na igizo dhima ili kuwajengea walimu tarajali maarifa ya kutosha.

(c) Wakufunzi wawahimize walimu tarajali kujisomea makala na machapisho mbalimbali na watoe mazoezi, majaribio na mitihani ya mara kwa mara ya ujirani au ukanda ili kuwajengea mbinu stahiki ya kujibu maswali yenye kupima umahiri.

*Kiambatisho A*

**MUHTASARI WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA SOMO LA URAIA**

| Na. | Mada | Namba ya Swali | Ufaulu katika kila Swali (%) | Wastani wa Ufaulu katika kila Mada (%) | Maoni |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Upimaji na Tathmini | 12 | 99.5 | 99.5 | Vizuri |
| 2. | Utamaduni Wetu | 3 | 93.2 | 97.4 | Vizuri |
| | | 7 | 99.0 | | |
| 3. | Uchambuzi wa Maandiko /Machapisho Muhimu ya Kufundishia Somo la Uraia | 11 | 93.2 | 96.5 | Vizuri |
| | | 14 | 99.8 | | |
| 4. | Maandalizi ya Kufundisha Somo la Uraia | 9 | 94.7 | 96.3 | Vizuri |
| | | 13 | 97.9 | | |
| 5. | Uchumi Wetu | 4 | 92.3 | 91.3 | Vizuri |
| | | 5 | 90.2 | | |
| 6. | Misingi ya Ufundishaji wa Somo la Uraia | 6 | 87.1 | 87.1 | Vizuri |
| 7. | Dola | 1 | 45.0 | 78.1 | Vizuri |
| | | 2 | 94.2 | | |
| | | 10 | 95.1 | | |
| 8. | Zana za Kufundishia na Kujifunzia | 8 | 66.1 | 66.1 | Wastani |

*Kiambatisho B*

**ULINGANIFU WA UFAULU WA WATAHINIWA KATIKA MADA KWA MWAKA 2022 NA 2023**

